**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Pakistan**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

**Jumamosi, 15 Safar 1445 H** **30/09/2023 M** **Na: 1445 / 11**

**<u>Taarifa kwa Vyombo vya Habari</u>**

# Uongozi wa Kijeshi na wa Kiraia Hebu na Uonywe. Kutambua Uwepo wa Umbile la Kiyahudi ni Khiyana kwa Mwenyezi Mungu (swt), Mtume Wake (Saw) na Waislamu. Watawala kama hao ni Wahalifu na Wanastahili Adhabu Kali Hapa Ulimwenguni na Kesho Akhera!

**(Imetafsiriwa)**

Mnamo tarehe 22 Septemba 2023, Waziri wa Mambo ya nje wa umbile la Kiyahudi, Eli Cohen alisema katika taarifa kwamba "nchi sita au saba" za Waslamu pia ziko tayari kusaini mikataba ya amani na umbile la Kiyahudi, kufuatia kujumuishwa kwa Saudi Arabia katika "makubaliano ya Abraham." "Amani na Saudi Arabia inamaanisha amani na ulimwengu mkubwa wa Kiislamu," alisema. Waziri wa Mambo ya nje wa Pakistan, Jalil Abbas Jilani, katika tweet moja, alitoa wito wa dola huru ya Palestina iliyojengwa, juu ya mipaka ya kabla ya 1967, wakati akizungumza juu ya suluhisho la dola mbili. Hili linaambatana sambamba na mpango wa Marekani, ingawa alidai ilikuwa kwa "maslahi yetu ya kitaifa." Mnamo tarehe 22 Septemba, 2023, ujumbe wa ngazi ya juu wa kijeshi kutoka Saudi Arabia ulikutana na Jenerali Asim Munir kujadili "maswala muhimu ya kikanda na kimataifa ya maslahi ya pande zote." Kwa hivyo, ni wazi kwamba wigo wa "Makubaliano ya Abraham," ambayo kwayo Imarati na Bahrain hapo awali zililitambua umbile la Kiyahudi, yanapanuliwa. Wachezaji wa kipindi kinachofuata cha usaliti, cha kuutambua uvamizi haramu wa Kiyahudi wa Palestina, ni watawala wa Saudia na nchi zengine za Waislamu.

Tunawaonya watawala wa kijeshi na kisiasa wa Pakistan kuachana na jaribio lolote kama hilo, au watu wa Pakistan watawahisabu. Waislamu wa Pakistan wanajua vyema uhalifu mwingi uliofanywa chini ya pazia la "maslahi ya kitaifa." Nchi hii iliundwa katika sehemu mbili kwa jina la maslahi ya kitaifa. Vikosi vya jeshi letu vilitumika nishati yao kwa ajili ya Vita vya Marekani. Kashmir alisalimishwa chini ya tishio la FATF. Sasa uhalalishaji wa usaliti wa ardhi ya Isra na Miraj utafanywa, kwa kutumia "maslahi ya kitaifa." Biashara hii chafu ni kwa badali ya uwekezaji unaowezekana wa dolari bilioni 70 hadi 100 kutoka Saudi Arabia, Imarati, Kuwait na Qatar.

Kuna suluhisho moja pekee kwa kadhia ya Palestina. Ni kuliangamiza umbile la Kiyahudi. Kila moja ya jeshi la nchi nyingi za Waislamu, ikiwemo Pakistan, Uturuki, Iran, Misri na Jordan, wana uwezo wa kufanya hivyo. Hili ndilo suluhisho sahihi pekee la Sharia. Mpango wa suluhisho la dola mbili ni mpango wa Marekani. Dola mbili inamaanisha kuutambua uvamizi haramu wa umbile la Kiyahudi kwenye nchi iliyobarikiwa ya Isra na Miraj. Hii ni ingawa ardhi hii na viunga vyake imebarikiwa na Mwenyezi Mungu ﷻ. Hakuna dola isiyo ya Waislamu iliyo na haki yoyote juu yake. Kwa hivyo, Waislamu nchini Pakistan wanapinga suluhisho lililojengwa juu ya mipaka ya kabla ya 1967, kwa sababu linatambua ukaliaji wa sehemu ya Palestina wa umbile la Kiyahudi. Kulipokuwa na Khilafah, Mayahudi hawakuweza kuikalia hata shubiri moja ya Palestina. Hata katika siku dhaifu zaidi za Khilafah Uthmani, Khalifa Abdul Hameed II hakuvumilia kutoa hata kipande cha ardhi ya Isra na Miraj kwa Mayahudi, kwa faida yoyote ya kidunia. Ardhi hii ilikombolewa kwa damu ya Maswahaba (ra) wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Walakini, baada ya kuibuka kwa tawala za kidikteta, ufalme na demokrasia katika ulimwengu wa Waislamu, Kibla chetu cha kwanza kimewekwa kwenye biashara duni.

Tunatoa wito kwa watoto wa Salah ud din al-Ayyubi katika vikosi vya jeshi la Pakistan kufuata nyayo za Salah ud din al-Ayyubi. Lazima waikomboe ardhi iliyobarikiwa ya Palestina kutoka kwa uvamizi muovu wa makafiri. Kwa kuongezea, Salah ud din al-Ayyubi kwanza aliunganisha Waislamu kufikia lengo hili. Kwa hivyo, lazima pia waungane na ulimwengu wa Waislamu kwa kutoa nusrah yao kwa Hizb ut tahrir kwa ajili kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Hatuhitaji hata vikosi vya jeshi la nchi "sita au saba" za Waislamu. Moja tu ni zaidi ya kutosha kuangamiza uvamizi wa Mayahudi. Hitajio la wakati huu ni kwamba majeshi ya Waislamu yaongozwe na Khalifa wa dhati, ambaye huhamasisha vikosi vyetu vilivyo tayari kwa ajili Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt).

**Enyi Vikosi vya jeshi la Pakistan!** Sio udhuru unaokubalika, mbele ya Mwenyezi Mungu (swt), kwamba mlikuwa tayari kwa ajili Jihad, lakini uongozi wenu na watawala walikuzuieni. Ni jukumu lenu la Sharia kuondoa kila kikwazo katika njia ya utabikishaji wa Sharia ya Mwenyezi Mungu na kutekeleza Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt). Hivyo basi jitokezeni na mutoe nusrah, nguvu na uwezo wenu, ili kuwapindua watawala wa Ulimwengu wa Waislamu na kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ]

**“Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”** [Surah At-Tawbah 9: 39].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Pakistan**

**Tovuti:** www.hizb-pakistan.com http://HizbPK.page.tl
**Pepe:** HTmediaPAK@gmail.com **WhatsApp: +90-531-814-7385**
**Twitter**: http://Twitter.com/HTmediaPAK **Facebook:** https://Facebook.com/HTmediaPAK10
**YouTube**: http://YouTube.com/HTmediaPAK **Dailymotion:** https://Dailymotion.com/HTmediaPAK

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info